RAMANI YA BIBLIA-“MPANGO WA MILELE WA MUNGU”



Ramani hii yaonyesha “Mpango wa Milele” wa Mungu, tangu jadi hadi jadi, kama ilivyonakiliwa katika neno lake ambalo limeandikwa, na kuvuviwa na Roho wake (2 Pet. 1:20,21).

Katika makusudi ya milele ya Mungu kunavyo vipindi 7 (Efe. 1:9,10). Katika kila moja ya vipindi hivyo mwanadamu alipewa wajibu au mtihani muhimu; lakini katika kila moja ya mitihani hiyo mwanadamu alianguka mtihani huo, jambo ambalo lilimletea hukumu. Basi matokeo ya mitihani hiyo yote ya vipindi hivyo 7 yalionyesha kwamba mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaa dhambi, kiumbe mpotevu kabisa (Rum. 3:10,23).

Na katika kila moja ya vipindi hivyo wokovu ulipatikana kwa NEEMA YAKE MUNGU (ikiwa ni kipawa ambacho mtu hastahili, na pia hafanyii kazi); na ulipatikana kwa njia ya IMANI. Mfano bora ni Habili (Waebrania 11:4); Henoko (5-6); Nuhu (7); Ibrahimu (8-19); Musa (23-29). Tazama pia Waefeso 2:8,9 na Warumi 6:23.

Kwa sasa sisi tunaishi katika kipindi cha nambari #6, kipindi cha Neema au cha Kanisa. Kipindi hiki kitakwisha wakati ambapo Kristo atakarudi ulimwenguni. Mwanzoni kabisa Yeye atarudi mawinguni kufufua ***WALIOKUFA NDANI YA KRISTO,*** na kubadilisha ***WANAOISHI KATIKA KRISTO*** na pia ***KUNYAKUA*** au kuwapokea ili wawe naye (Yoh. 14:1-3; 1 Thes. 4:16,17). Jambo hili laweza kutokea ***HIVI KARIBUNI*** –hebu zingatia mkusanyiko tena wa taifa la Israeli – ***KWA GHAFLA*** (1 Kor. 15:52), na ***KUWATENGANISHA*** walio-oko-ka (waliozaliwa mara ya pili, katika Kristo; Yoh. 3:6,7; Rum. 8:1,9) kutoka kwa wale ambao hawajaokoka. Wale ambao wanasikia ukweli wa Injili wanahakikishiwa na Roho Mtakatifu na kumwamini Kristo ili wapate kuokoka, lakini wanaokataa na kutomkubali Kristo baada ya Unyakuzi watakuwa chini ya himaya na udanganyifu wa Mpinga Kristo na watapata hukumu ya milele (2 Thes. 2:10-12; Ufu. 13:14-18; 14:9-11). Baada ya kipindi cha Mateso Kristo atarudi duniani katika utukufu wake ili kuleta Ufalme wake wa miaka 1,000 (Mat. 24:29,30; Ufu. 19:11—20:6; Yuda 14,15).

Mateso ambayo yatakuwako yatakuwa yametoka-na na hukumu yake Mungu kwa ulimwengu ambao umemkataa Kristo, nao wanadamu wataomba milima iwaangukie na kuwaficha (Ufu. 6:12-17). Kutakuwa na vita vingi na ***ANGALAU NUSU YA WATU WOTE ULIMWENGUNI WATAUAWA*** (Ufu. 6:4,8; 9:15-18)! Wanadamu watachomeka kwa moto na kutakuwa na mitetemeko mikuu ya ardhi na mvua kubwa ya mawe. Miji mikubwa itaangushwa na kila kisiwa na mlima vitatokomea, hapo wakati baada ya ***KUNYAKULIWA*** kwa kanisa (Ufu. 3:10; 16:8-9, 18-21).

Kiti Cheupe cha Enzi ya Mungu kitakuwa ndicho hukumu ya mwisho ya Mungu kwa wote ambao wamekataa NEEMA yake, waliokataa wokovu wake unaopatikana kwa IMANI. Watu hao wote wa vizazi vyote watafufuliwa, watahukumiwa, halafu watatupwa kwenye Tanuri la Moto ambako watadumu milele (Ufu. 20:11-15).

HEBU SASA TUWEZE KUULIZA MASWALI MAWILI

#1. Je, kama kunyakuliwa kungefanyika leo wewe utanyakuli-wa?

#2. Je, ungalipenda kujua kwamba utakuwa na Kristo wakati huo?

KAMA UNGEPENDA HIVYO TAFADHALI JIBU MAS-WALI AMBAYO YANAPATIKANA KATIKA UPANDE WA NYUMA WA JALIDA HILI . . .

Kwa sababu sasa umetazama “Ramani ya Biblia” na mambo ya-takayokuja, HATMA YAKO NI IPI?
Hebu chunguza moyo wako kwa ukweli, HALAFU UWEKE ALAMA AU UANDIKE JIBU LAKO LA KWELI.

1.Je, unaamini kwamba wote wametenda dhambi dhidi yake Mungu na wanahitaji kuokoka? NDIO ---- LA ----.
2. Je, una TASHWISHI ------, WADHANI -------- AU WAJUA -------- kwamba SASA una uzima wa milele na kwamba unaelekea mbinguni?
3. KWA KWELI wewe unatarajia kupata wokovu WAKO kwa njia gani (kwa kulipia dhambi zako ili uweze kufika mbinguni)?
A. KUPITIA KWAJUHUDI ZA KIBINADAMU, useme:

	NDIO	HAPANA
“Kuishi maisha mazuri”	----------	----------
“Kutenda matendo mema	----------	----------
“Kuwa mshirika wa kanisa”	----------	----------

B. NJIA NYINGINE (itaje kwa njia ya moja kwa moja) ----------
4. Ni asilimia (%) ipi ya tumaini lako la kupata wokovu liko katika:

A. JUHUDI ZA KIBINADAMU ---------- B. KWA NJIA ZINGINE ----------
(Kwa mfano: 50/50, 70/30, 100/0, n.k.)

SASA CHUNGUZA MAJIBU YAKO KWA MASWALI YALIYOKO HAPO JUU UKILINGANISHA NA MAANDIKO YAFUATAYO:

#1. Watu wengi hujibu swali la 1 “NDIO”. Jibu hili liko sawa kwa sababu Neno la Mungu linasema:

> Watu WOTE wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wake Mungu – gharama ya dhambi ni MAUTI (kutenganishwa na Mungu kwa SASA
> na kwa MILELE).
> (Rum. 3:23; 6:23; Efe. 2:5; Ufu. 20:14; 21:8).

Je, ni NANI wametenda dhambi dhidi ya Mungu na wanahitaji kuokolewa kutokana na KIFO? Watu fulani ---------, watu Wengi ----- au watu Wote, Je, na wewe ----------.

#2. Watu wengi hujibu swali la pili “WADHANI”, lakini sasa nina HABARI NJEMA kwako! Mungu anasema:

> NIMEWAANDIKIA ninyi mambo (ahadi) hayo,
> ili MJUE ya kuwa mna uzima wa milele (1 Yohana 5:13).

Je, Mungu angetaka wewe ujue kwamba una uzima wa milele? NDIO ------- HAPANA ----------.
Je, ni kitu gani ambacho Mungu amekupatia ili uweze kujua jambo hilo? Hisia zako ---------- au Neno (Biblia) lake lililoandikwa ----

#3. Watu wengi hujibu swali la 3 “NDIO”. Tumaini lao liko katika juhudi zao ZA KIBINADAMU ili waweze KUSTAHILI KUPATA wokovu wao. Lakini Neno la Mungu lasema:

> Utakatifu wetu wote (juhudi zetu za kibinadamu za kupata wokovu) ni kama “NGUO ILIYOTIWA UNAJISI” (Isa. 64:6).

Je, wajua ni KWA NINI Mungu huona kwamba bidii zetu za kibinadamu, matendo yetu mema n.k. ya kuupata wokovu ni “nguo iliyotiwa unajisi”? NDIO ----- LA ----- Ni kwa sababu Neno lake lasema:

> Kristo ALIKUFA KWA AJILI YA DHAMBI ZETU, kama yanenavyo maandiko – na kufufuka tean (1 Kor. 15:3,4).

BASI tunapojaribu kufanyia wokovu wetu kazi basi hapo huwa **TUNAKATAA** kifo chake Kristo ambacho **TAYARI KISHALIPA** kwa ajili yadhambi na wokovu wetu.
Je, sisi tunastahili **KUKATAA** malipo **YAKE** ya dhambi zetu na kujaribu kufanya kazi ili kustahili wokovu wetu?
NDIO ------ LA -------.

HEBU KWA SASA TUTAZAME JINSI AMBAVYO MUNGU AMESEMA KWAMBA TUMEOKOKA:

> Kwa maana mmeokolewa kwa NEEMA (rehema), kwa njia ya IMANI; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni KIPAWA cha Mungu wala SI KWA MATENDO
> (Efe. 2:8,9).

Je, wajua maana ya NEEMA? NDIO ----- LA ---- (rehema ambazo hatustahili, kinyume na sisi kupata haki).
Je, waweza KUFANYIA zawadi kazi? NDIO ------ LA -----. Je, tunapokeaje KIPAWA cha Mungu cha wokovu? Kwa kuipokea kwa imani ---- au kwa kuistahili kwa njia ya kutenda matendo mema? ------

NA JE, MATENDO MEMA YANAINGIA VIPI KATIKA MPANGO WAKE MUNGU?

Matendo mema yanahitaji KUFUATA au kuwa matokeo ya wokovu (Efe. 2:10). Hayo yanastahili kuwa njia ya mtu kusema ASANTE kwa MUNGU kwa ajili ya kupewa KIPAWA chake cha Wokovu.
JE, JUHUDI ZA KIBINADAMU ZIZAWEZA KUMFANYA MTU KUSTAHILI KUPATA WOKOVU? NDIO ------ LA ----- . . . NDIO, KWA KIWANGO KIDOGO ----------.

#4. Watu wengi hujibu swali la 4 kwamba wao hawamtumaini Yesu Kristo PEKE YAKE (asilimia 100%) kwa ajili ya wokovu wao. Lakini hebu tazama jinsi Neno la Mungu linavyosema:

> Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika MWANAWE. YEYE ALIYE NA MWANA anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima (1 Yoh. 5:11,12).

Je, wewe huna budi KUWA PAMOJA NA NANI kama Mwokozi wako ili kuweza kupata uzima wa milele? (Chora mstari chini ya jibu lako kuonyesha jibu lako katika andiko lililonukuliwa hapo juu).
Je, ni asilimia (%) gani ya tumaini lako la wokovu LINASTAHILI kuwa katika jitihada za kibinadamu? ----- Na Katika Kristo? ----------

SASA hebu tutazame JINSI unaweza kupata uzima wa milele katika Yesu Kristo na KUJUA jambo hilo kwa njia ya USHAHIDI.

> AMWAMINIYE (kumtumaini, kumtegemea) MWANA YUNA (mara moja anapata) UZIMA WA MILELE; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali GHADHABU YA MUNGU inamkalia (Yohana 3:36).

Je, utapata nini kama **UTAMWAMINI** (kumtumaini, kumtegemea) Kristo? (Chora mstari chini ya jibu lako katika andiko lililoko hapo juu).
Je, usipokuwa na Kristo utapata nini? (Pia chora mstari chini ya jibu lako).

JE, WEWE UTAMWITIKAJE KRISTO SASA?

Je, unatambua kwamba BWANA Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zako na akafufuka tena? NDIO ------ LA ----------.

JE, WEWE UTAWEKA TUMAINI LAKO LOTE (100%) KATIKA BWANA YESU KRISTO KWA AJILI YA WOKOVU WAKO SASA? NDIO ---------- LA ------.

Je, ni kitu gani ambacho wewe nacho sasa? Uzima wa milele ---------- au ghadhabu yake Mungu ---------- na WALIJUAJE JAMBO HILO?
(Tazama andiko la Yohana 3:36 lililopo hapo juu) ----------

Je, kwa SASA wewe unatumaini nini ili upate wokovu wako? Bidii au jitihada zako -----, Kristo ----- au zote mbili ----------.

JE, SASA UNGEPENDA KUMSHUKURU MUNGU KWA AJILI YA WOKOVU WAKO KUPITIA KWA YESU KRISTO?

TAREHE ---------- SAHIHI YAKO ----------.

For current ordering and contact information please go to www.bbea.org

Several langages and items may be freely downloaded worldwide at www.bbea.org
in the USA, you may also request a free “Track Sample Pack” and your choice of other items
free at www.bbea.org

RAMANI YA BIBLIA

Kimeandikwa na Leon Bates

PIA: KUNA MASWALI KUHUSU HATMA YAKO